BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru Mweneyzi Mungu muumba mbingu na ardhi na kila kilichomo ndani yake NA kutuwezesha kukutana tena katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria tukiwa wazima wa afya ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi katika Mkutano huu wa Bajeti kwa kujadili, kushauri na hatimae kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wao wa kufanya maamuzi ya hekima na busara ya kutengeneza filamu ya ***'ROYAL TOUR'*** kwa lengo la kuimarisha sekta ya Utalii. Tunaamini kuwa matunda ya filamu ile yatasaidia kwa namna ya kipekee kuinua utalii wetu na hatimae kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo na mabadiliko chanya katika sekta ya Utalii. Aidha, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inachukua nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza kwa dhati aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mheshimiwa Lela Mohammed Mussa kwa mashirikiano yake makubwa aliyoipatia Kamati hii katika kipindi chote cha uongozi wake, tunamtakia kila la kheri katika majukumu mapya katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunaamini kuwa atayaendeleza yale yote mazuri aliyokua akiyafanya katika Wizara hii kwa lengo la kuiletea sekta ya elimu mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee kabisa naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa jinsi walivyojitoa kwa hali na mali kwa lengo la kuisaidia Serikali kutimiza malengo yake kwa wananchi kwa michango yao mizuri pamoja na uchambuzi wa kina walioufanya kuhusiana na bajeti hii. Michango na maoni yao imesaidia sana katika uandaaji wa hotuba hii pamoja na kuisaidia Wizara kurekebisha pale ambapo Wajumbe walielekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba niwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi — Mwenyekiti
2. Mhe. Azza Januari Joseph — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanajuma Kassim Makame — Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali — Mjumbe
5. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa — Mjumbe
6. Mhe. Said Saleh Salim — Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir — Katibu
8. Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri — Katibu

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua nchi yetu ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizojaaliwa kuwa na idadi kubwa ya vivutio vingi vya asili pamoja na maeneo mengi ya kihistoria ambayo kwa namna ya kipekee huwavutia watalii kutoka maeneo mbali mbali duniani. Kamati inaamini kuwa, vivutio hivyo vikilindwa na vikiimarishwa ipasavyo vitazidisha fursa ya kuongeza pato la taifa pamoja na kuwasaidia wananchi wetu kwa kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo ya Serikali katika utekelezaji wa programu zilizopangwa ndani ya bajeti hii yanafikiwa, Kamati inaamini kuwa malengo hayo yatafanikiwa endapo tu fedha zilizotengwa ndani ya bajeti tunayotegemea kuipitisha hapa zinapatikana kwa wakati. Kamati inayasema hayo kutokana na uzowefu wa bajeti iliyopita ambapo baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ilipangwa kutekelezwa katika mwaka huo wa fedha haijakamilika mpaka sasa kutokana na ukosefu wa fedha. Kamati inashangazwa na hali hiyo ambapo tunaamini kuwa wakati tunapitisha bajeti tulipanga kwa kujua fedha zipo na zitapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilianza kupitia bajeti ya Wizara hii kwa kuangalia mapato ya Wizara na taasisi zake mbali mbali ambazo zinakusanya mapato. Kwa kiasi kikubwa Kamati haikuridhika na ukusanyaji wa mapato kwa baadhi ya taasisi ambapo Ofisi Kuu Pemba mapato yaliyokusanywa kutoka mwezi Julai 2020 hadi Machi 2021 yalikuwa ni 13% tu zilizokusanywa. Sababu mbali mbali zilielezwa mbele ya Kamati za kushuka kwa mapato hayo ikiwemo ya kukosekana kwa watalii wa kutosha kisiwani Pemba sababu ambayo inakubalika kutokana na hali halisi ilivyo kwa sasa. Hata hivyo, Kamati inachukua nafasi hii kuiomba Wizara ya Fedha inapopanga mapato kwa taasisi mbali mbali iangalie na uhalisia na uwezo wa vyanzo vya mapato. Kamati inayasemsa hayo kutokana na kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa taasisi nyingi ukiachia na hii tuliyoitakja iliyopo katika Wizara hii, lakini jambo hili hata katika Wizara nyengine lipo, hivyo tunaomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na mapato ya Mamlaka ya Mji Mkongwe ambapo kutoka mwezi Julai 2020 hadi Machi 2021 mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mji Mkongwe yalikua ni shilingi **68,605,000.00** sawa na **76.23%** na Kamisheni ya Utalii nayo ilikusanya shilingi **4,038,856,920** sawa na **72.45%.** Tunazipongeza taasisi hizi na tunaziomba ziendeleze juhudi za kukusanya kwa lengo la kunyanyua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ilipitisha bajeti ya Wizara hii kwa kutoa maelekezo na ushauri kidogo ambao Wizara iliahidi kuufanyia kazi ili malengo ya mwaka huu wa kibajeti yaweze kukamilika kwa wakati. Kwa mwaka 2022/2023 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza Programu kuu tano kama zifuatazo:-

i) Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii;

ii) Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

iii) Programu ya Utawala na Uendeshaji;

iv) Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii; na

v) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii.

PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

Mheshimiwa Spika, Programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi kwa kuzingatia kuwa imelenga katika kuweka mazingira bora ya rasilimali watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango katika sekta nzima ya utalii.

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni, Serikali imezindua kikosi cha Polisi wa Utalii na Diplomasia kwa lengo kuimarisha hali ya usalama katika sekta nzima ya utalii pamoja na kutekeleza ahadi ilizozitioa awali kwa wananchi katika sekta hiyo. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa uzinduzi wake huo na inaahidi kutoa ushirikiano wa hali na mali. Tunaamini kuwa, uwepo wa kikosi hicho utasaidia sana kupunguza matukio mbali mbali ya uhalifu katika utalii ambayo yalikua yanaitia dosari nchi yetu. Ili kikosi hiki kiweze kufanikiwa kinahitaji kuwezeshwa kwa mahitaji yote yanayotakiwa kwa walinzi hao ambao kwa sasa wapo maafisa 150 ambao wanatakiwa kutimiziwa mahitaji yao yote.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliweka malengo katika sekta ya utalii ya kuongeza idadi ya wageni wanaoitembelea Zanzibar kutoka **538,264** mwaka 2019 hadi kufikia wageni **850,000** mwaka 2025. Kamati inaamini kuwa jambo hilo litafanikiwa endapo mipango yote ya utekelezaji wa programu za Wizara itafuatwa kama ilivyopangwa pamoja na upatikanaji wa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa tunaweza kufikia malengo hayo kwa kuhakikisha kuwa yale maeneo ya kihistoria tuliyoyaimarisha yanafanya kazi kwa kuhamasisha watalii kuyatembelea maeneo hayo pamoja na kuyatangaza kwa kadri tunavyoweza. Aidha, tunaamini kuwa utalii wa ndani nao ni miongoni mwa vipaumbele ambavyo Wizara inatakiwa ivitilie mkazo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya Utalii kwa wote iliyoanzishwa na awamu iliyopita ilikua na lengo la kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na sekta ya utalii moja kwa moja kwa kuwahamasisha wananchi kuwekeza katika sekta ya utalii. Lengo hili litafikiwa endapo tu Kamisheni ya Utalii na Idara nyengine husika zitapatiwa fedha za kutosha kutimiza wajibu wao.

Mheshmiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi **654,042,,000** fedha ambazo zimeongezeka kidogo ukilinagnisha na bajeti

iliyopita ambapo makadirio kwa mwaka 2021/2022 zilikuwa ni shilingi **595,510,000** fedha ambazo hazikupatikana zote katika utekelezaji wake.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

Mheshimiwa Spika, Programu hii imelenga kuhifadhi, kuimarisha na kuendeleza maeneo yote ya kihistoria pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa wananchi wote. Lengo la Serikali kwa sasa ni kuona kuwa wananchi na jamii nzima wananufaika na sekta utalii. Aidha, jamii itapata fursa ya kuuelewa utalii wenyewe na kufanya juhudi za kuyalinda na kuyathamini maeneo ya kihistoria ukiwemo Mji Mkongwe ambao umepata umaarufu duniani kote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya juhudi mbali mbali za kuhakikisha kuwa haiba ya Mji Mkongwe inarejea kwa kufanya ukarabati wa maeneo mbali mbali katika eneo hilo pamoja na kuyakodisha baadhi ya majengo kwa makubaliano ambayo Serikali itanufaika. Pamoja na hatua nzuri hizo zinazochukuliwa bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinarudisha nyuma juhudi hizo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa fedha za kukamilisha baadhi ya miradi ya maendeleo ukiwemo mradi wa ujenzi wa Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe hai.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuimarisha Makumbusho ya Viumbe Hai na Makumbusho ya Amani una gharama ya shilingi **769,605,546** na hadi Kamati inapokea taarifa ya Wizara wakati wa kupitisha bajeti ilielezwa kuwa mjenzi alikwishapatiwa shilingi **125,327,883.61** sawa na 16%. Kusuasua kwa mradi huu kunatoa picha halisi kuwa juhudi zinazochukuliwa kwa sasa hazitoweza kukamilika kwa asilimia mia moja. Kamati inasikitishwa sana kuona kuwa Serikali inapanga mipango mizuri katika kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa lengo la kuunyanyua uitalii nchini lakini ukosefu wa fedha kwa wakati ni jambo linalorudisha nyuma juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii imekadiriwa jumla ya shilingi **9,988,480,000** ambazo zitatumika katika maeneo mbali mbali kama yalivyoelezwa na Wizara katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Makadirio hayo yameongezeka kwa mwaka huu ukilinganisha na makadirio ya mwaka uliopita ambayo yalikua ni shilingi **6,115,154,000.** Pamoja na ongezeko hilo, Kamati inasisitiza kuwa kutokana na miradi mingi ya kimkakati kukwama utekelezaji wake katika bajeti iliyopita kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za ukosefu wa fedha kwa wakati, tunaishauri Serikali kwa bajeti hii tunayoipitisha fedha zake zipatikane kwa wakati ili ile athari ya

utekelezaji wa miradi hiyo iweze kuonekana na wananchi wanufaike na matunda ya Utalii kutokana na juhudi zao za kuyalinda maeneo ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, kupitia bajeti hii tunapenda kuishauri Serikali na Wizara kwa ujumla kupitia taasisi zake kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya suala zima la uhifadhi wa maeneo ya kihistoria. Katika ziara za Kamati katika baadhi ya maeneo, Kamati ilibaini changamoto ya baadhi ya wananchi kufanya uharibifu mkubwa wa maeneo ya kihistoria hasa wale wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo.

PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

Mheshimiwa Spika, programu hii inabeba mambo mengi ya msingi yakiwemo ya kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti mbalimbali pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale, kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara na kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara Ofisi Kuu Pemba.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii watendaji wanapaswa kuwa makini kutokana na ukweli kwamba shughuli zote zilizopo katika programu hii, ndizo zitakazoleta matokeo mazuri ya utekelezaji wa programu zote. Kutokana na hali hiyo, tunasisitiza umakini wa Wizara ili utekelezaji wa malengo yaliyopangwa uweze kufanikiwa. Aidha, Kamati inachukua nafasi hii kuiomba Serikali kuziingiza fedha zote kwa wakati kama zilivyoombwa ili kilichopangwa kiweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/2023 programu hii imekadiriwa kutumia shilingi **2,775,713,000** ambapo kwa mwaka uliopita wa 2021/2022 ilikadiriwa jumla ya shilingi **2,447,061,000** . Kamati imefurahishwa na uongezekaji wa makadirio hayo kwa mwaka huu na inaiomba Serikali kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapatikana kwa wakati ili utekelezaji ufanyike kama ulivyopangwa.

KAMISHENI YA UTALII

Mheshmiwa Spika, Kamisheni ya Utalii ina jukumu la kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa dhana ya Utalii kwa wote inafikiwa na faida kwa wananchi inapatikana.

Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Utalii katika utekelezaji wa malengo yake ina programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii.

PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wananchi na jamii ya kimataifa kuhusiana na bidhaa na huduma za utalii zilizopo nchini. Programu hii inalenga katika kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii duniani kote. Aidha, programu inalenga kuongeza idadi ya watalii kwa kuwawekea mazingira mazuri yatakayowavutia na kuwahamasisha kuingia kwa wingi nchini. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko.

Mheshimiwa Spika, katika lengo lile lile la kuutangaza utalii, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi, wamefanya kazi kubwa ya kuutangaza utalii wetu kwa kutengeneza filamu ya **'ROYAL TOUR'** iliyolenga kuvitangaza duniani vivutio vya utalii, utamaduni na fursa za uwekezaji zilizopo hapa nchini. Filamu ya ***'Royal Tour'*** ilianza kurekodiwa Agosti 29, 2021 na muongozaji wa filamu hiyo ni Bwana Peter Greenberg aliyeambatana na Rais Samia kutembelea vivutio mbalimbali ukiwemo Mji Mkongwe, fukwe za bahari na hifadhi za Taifa zinazopatikana Tanzania Bara. Kupitia filamu hiyo, Tanzania na Zanzibar muda mchache ujao zitaweza kupata fursa ya uwekezaji mkubwa kutoka kwa makampuni na wadau mbali mbali duniani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa kazi zinazofanywa na maraisi wetu zitaweza kuleta tija zaidi endapo Kamisheni na Wizara zitafanya jitihada za makusudi za kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusiana na huduma zinazopatikana katika sekta nzima ya Utalii. Ni vyema idara ya masoko inapoandaa mikakati ya kuitangaza nchi yetu kwa kuandaa matamasha mbali mbali na maonyesho ya kibiashara ikawashirikisha wananchi moja kwa moja ili wananchi hao wazidi kuhamasika na kuitangaza nchi yetu katika maeneo ambayo pengine Kamisheni haikuyafikia.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya maeneo ya kitalii miundombinu yake hairidhishi, hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa lengo la kuijenga miundombinu ya barabara ambapo nyingi miongoni mwa barabara hizo ni mbovu sana jambo linaloathiri moja kwa moja sekta ya utalii. Katika hotuba ya Kamati yetu kwa Bajeti iliyopita, tulileta ombi hili ambalo bado halijafanyiwa kazi kwa sababu katika maeneo mengi ya utalii ambayo Kamati imeyatembelea miundombinu yake bado hairidhishi. Hivyo, tunalileta tena ombi hili kwa Serikali na tunaiomba ilitilie mkazo suala hili kwa kuzijenga barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya programu hii yataonekana kupitia ongezeko la idadi ya watalii wanaoingia nchini, hivyo ni vyema bajeti inapopangwa iangalie na shughuli mahususi zinazopangwa ili yale malengo yanayopangwa yaweze kukamilika. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi

654,042,000 ambapo kwa mwaka ulipita wa 2021/2022 programu hii ilikadiriwa umla ya shilingi **595,510,000.**

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAMISHENI YA UTALII

Mheshimiwa Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu katika sekta ya utalii pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Kamisheni ya Utalii.

Mheshmiwa Spika, mafunzo kwa wafanyakazi na watoa huduma wa sekta ya utalii ni muhimu hivyo, katika utekelezaji wa programu hii, Kamati inashauri wahusika hao wa sekta ya utalii wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri na kwa ufanisi. Aidha tunashauri mafunzo hayo yatolewa kwa kuzingatia ukubwa wa majukumu na kuwashirikisha wafanyakazi wote wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ya mwaka huu wa 2022/2023 kwa programu hii ni shilingi **3,219,559,000** ambapo mwaka uliopita wa 2021/2022 makadirio yalikuwa ni shilingi **1,447,390,000.** Kwa mwaka huu wa fedha, makadirio yameongezeka na tunapongeza ongezeko hilo. Tunaiomba Serikali ihakikishe kuwa fedha hizo zinapatikana kwa wakati ili mpango kazi na malengo yaliyopangwa katika programu hii yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa, upatikanaji wa fedha kwa wakati ni muarubaini tosha wa utekelezaji wa malengo yote yaliyopangwa na Wizara. Naomba nichukue nafasi hii kluwaomba Wajumbe wenzangu waendelee kupaza sauti kuhusiana na jambo hili, ili Serikali isikie na ijitahidi kutoa fedha kwa wakati. .

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuihamasisha Kamisheni ya Utalii kuendelea na jukumu lake la msingi la kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi kwa kubuni vyanzo vyengine vya masoko ambavyo vitakubalika kitaifa kwa lengo la kuongeza pato la taifa.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika Baraza lako tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao pale panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



.....

Yussuf Hassan Iddi,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.